# Kubadilisha waajiri nchini Qatar

## Habari muhimu kwa wafanyakazi

State of Qatar
MINISTRY OF LABOUR

Wafanyakazi wote katika Jimbo la Qatar wanaweza kubadilisha kazi bila ya kupata Cheti cha Hakuna Pingamizi (NOC) wakati wowote katika kipindi cha mkataba wao.

Ilhali kuondolewa kwa NOC kunawahusu wafanyakazi wote, sheria za kusitisha mkataba wa ajira na kubadilisha kazi zinatofautiana kufuatana na makundi mbalimbali ya wafanyakazi.

**KAMA UNAFANYA KAZI KATIKA SEKTA BINAFSI AMBAYESHERIA YA KAZI NAMBA. 14 YA 2004 INAKUHUSU**

## Je, ninapaswa kufuata utaratibu gani kubadilisha kazi?

1. Unahitaji kutuma maombi ya kubadilisha kazi kupitia mfumo wa arifa wa kielektroniki wa Wizara ya Kazi (MoL). Nenda kwenye tovuti ya Wizara na uchapishe nakala ya fomu ya "Badilisha Mwajiri". Jaza fomu na taarifa zote zilizoombwa kuhusu wewe na kuhusu mwajiri wako mpya, kisha utie saini. Pia mwombe mwajiri wako mpya aweke muhuri rasmi wa kampuni na aisaini fomu hiyo.
2. Piga picha au skani fomu iliyojazwa na kutiwa saini, na uingie kwenye mfumo wa arifa wa kielektroniki wa MoL ukitumia nambari yako ya Kitambulisho cha Qatari (QID) na nambari yako ya simu ya mkononi. Kumbuka nambari ya simu ya mkononi unayotumia kuingia lazima iunganishwe na QID yako. Mara tu unapoingia kwenye mfumo, pakia fomu ya "Badilisha Mwajiri" iliyojazwa na kutiwa saini.
3. Mara tu unapotuma maombi yako, mfumo utatoa nambari ya EC (Badilisha Mwajiri) ambayo itaonekana kwenye skrini yako. Nambari ya EC ni muhimu sana, kwa hiyo hakikisha umeiandika, umeipiga picha kwa simu yako.
4. Mara tu ombi lako la kubadilisha kazi litakapoidhinishwa na Wizara, utapokea ujumbe mfupi wa simu kutoka Wizara ikithibitisha mabadiliko yako ya kazi na kukujulisha kuhusu kipindi chako cha notisi. Mwajiri wako wa sasa na mwajiri wako mpya pia watapokea ujumbe mfupi wa simu.
   - Iwapo umefanya kazi na mwajiri wako wa sasa kwa miaka miwili au kwa muda usiozidi huo, kipindi cha notisi yako kitakuwa **mwezi 1.**
   - Iwapo umefanya kazi na mwajiri wako wa sasa kwa zaidi ya miaka miwili, kipindi cha notisi yako kitakuwa **miezi 2.**

   Mwisho wa kipindi cha notisi yako kitaonyeshwa kwenye ujumbe mfupi wa simu kutoka kwa wizara. Inabidi uendelee kufanya kazi kwa mwajiri wako wa sasa katika kipindi hiki cha notisi.
5. Ndani ya miezi mitatu kuanzia mwisho wa kipindi chako cha notisi, mwajiri wako mpya atalazimika kutuma maelezo ya mkataba wako wa ajira kupitia Mfumo wa Uthibitisho wa Kidigitali wa MoL kwa Mkataba wa Ajira wa Lugha Nyingi. Hii itatoa mkataba wako mpya wa ajira, ambao wewe na mwajiri wako mpya mnahitaji kuutia saini. Mara tu utakapokuwa umetiwa saini na nyote wawili, mwajiri mpya ataipakia kwenye jukwaa la kidigitali la MoL kwa ajili ya uthibitishaji. Mwajiri wako mpya lazima akupe nakala ya mkataba ulioidhinishwa na MoL. Unaweza pia kuipakua kutoka kwenye tovuti ya MoL.
6. Hatimaye, mwajiri wako mpya ataingia kwenye ukurasa wa tovuti ya Wizara ya Mambo ya Ndani wa huduma za Metrash ili kukuombea QID mpya. Mwajiri wako mpya lazima akupe QID mpya.

## Je, ni lazima nifuate utaratibu uleule wa kubadilisha kazi katika kipindi changu cha majaribio?

Inaweza kubainishwa katika mkataba wako wa ajira kwamba utakuwa chini ya kipindi cha majaribio kilichokubaliwa na mwajiri wako. Hata hivyo, kipindi hiki cha majaribio lazima kisizidi miezi sita tangu tarehe ya kuanza kwa kazi yako, na huwezi kuwa chini ya kipindi cha majaribio zaidi ya kimoja na mwajiri huyo huyo.

Unaweza kusitisha mkataba wa ajira ndani ya kipindi cha majaribio, ilimradi unatii yafuatayo:

- Tuma ombi lako la kubadilisha kazi kupitia mfumo wa arifa wa kielektroniki wa MoL kama ilivyoelezwa hapo juu angalau mwezi mmoja kabla ya kupanga kuacha kazi yako.
- Mwajiri wako mpya lazima amlipe fidia mwajiri wako wa sasa sehemu ya ada za uajiri na tikiti ya ndege ya safari ya kwenda tu kwa kiwango ambacho kilikubaliwa na waajiri wa sasa na wapya, ingawa kisichozidi miezi miwili ya mshahara wako wa msingi wa sasa.
- Baada baada ya idhini ya Wizara yakubadilisha kazi, utapokea ujumbe mfupi wa simu kutoka MoL ukithibitisha mabadiliko yako ya kazi na kukuarifu kuhusu kipindi chako cha notisi. Tarehe ya mwisho ya kipindi chako cha notisi itaonyeshwa kwenye ujumbe mfupi wa simu. Ni lazima uendelee kufanya kazi na mwajiri wako wa sasa hadi tarehe ya mwisho isipokuwa kama mmekubaliana vinginevyo na mwajiri wako wa sasa.

## Ninawezaje kuangalia hali ya ombi lililowasilishwa kwa mfumo wa arifa wa kielektroniki wa MoL?

Mara tu unapotuma ombi lako la kubadilisha kazi kwa kutumia mfumo wa arifa wa kielektroniki wa MoL, unaweza kuangalia hali ya ombi kupitia kiunganishi kifuatacho: http://ecai.adlsa.gov.qa/
Ili kuingia, utahitaji kujumuisha nambari yako ya QID na nambari ya EC iliyotolewa na mfumo wa arifa wa kielektroniki wa MoL wakati ulipotuma ombi lako.

## Nini kitatokea ikiwa sitakamilisha kipindi cha notisi na mwajiri wangu wa sasa?

Ukiamua kuacha kufanya kazi kabla ya mwisho wa kipindi chako cha notisi, utalazimika kumlipa mwajiri wako wa sasa kila siku ya kipindi cha notisi ambacho hufanyi kazi.

Hii inahesabiwa kama kiasi sawa na mshahara wako wa kimsingi kwa sehemu iliyobaki ya kipindi cha notisi kwa msingi sawia. Kwa mfano: Ikiwa unataka kuacha kufanya kazi wiki mbili kabla ya kumalizika kwa kipindi chako cha notisi na mshahara wako wa msingi ni QAR 1,500 kwa mwezi, utalazimika kumlipa mwajiri wako QAR 750 ili kusitisha mkataba kisheria.

## Je, ninaweza kukubaliana na mwajiri wangu wa sasa kutotimiza kipindi changu cha notisi?

Ndio, wewe na mwajiri wako wa sasa mnaweza kukubaliana kutotimiza kipindi cha notisi. Katika hali kama hiyo, unaweza kuambatisha barua iliyotiwa saini na wewe na mwajiri wako wa sasa kwa ombi lako la kubadilisha kazi. Barua iliyotiwa saini inapaswa kutambua wazi wazi kwamba wewe na mwajiri wako wa sasa mmekubaliana kutozingatia kipindi cha notisi kilichofafanuliwa na sheria husika. MoL itazingatia makubaliano ya pande zote wakati wa kubainisha kipindi cha notisi.

## Je, ninahitaji kumlipa au kumgharimia mwajiri wangu mpya kwa ajili ya gharama yoyote ya kiutawala kwa badilko hilo la mwajiri?

Hapana, utaratibu wa kubadilisha mwajiri ni bure kwa wafanyakazi. Vilevile, **huhitaji** kulipa au kugharimia kiasi chochote kwa mwajiri wako mpya kwa ajili ya utoaji wa QID mpya.

## Je, mwajiri wangu wa sasa anaweza kughairi QID yangu baada ya kutuma ombi langu la kubadilisha kazi?

Mara unapokuwa umetuma ombi lako la kubadilisha kazi kupitia mfumo wa arifa wa kielektroniki wa MoL, mwajiri wako wa sasa hawezi kughairi QID yako au kuwasilisha kesi ya uongo ya kutoroka.

## What can I do if my current employer cancels my QID before I submit my application to change jobs?

Iwapo mwajiri wako wa sasa ataghairi QID yako kabla ya kutuma ombi lako basi unahitaji kwanza kutuma lalamiko aidha kupitia Jukwaa La Pamoja la Malalamiko na Wakosoaji wa Serikali la MoL au kwa kwenda MoL. Baada ya Wizara kukagua lalamiko lako, itabidi utume barua iliyotiwa saini kwa Kiarabu iliyotumwa kwa Mkuu wa Idara ya Mahusiano ya Kazi ikiomba kuanzisha upya QID yako. Katika barua, unapswa kujumuisha maelezo mafupi kwa nini unaomba QID yako ianzishwe upya. Hakikisha umetaja nambari zako za QID na za simu ya mkononi kwenye barua. Mbali na barua iliyotiwa saini, unapaswa pia kutuma nakala ya QID yako, nakala ya ujumbe mfupi wa simu inayoarifu kuhusu kughairiwa kwa QID yako; na nakala ya ofa mpya ya kazi. Kumbuka kuweka nakala ya hati hizi kwa ajili ya kumbukumbu yako.

MoL itashirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ili kuanzisha upya QID yako. Unaweza kuangalia hali ya QID yako kupitia Metrash.

Mara QID yako itakapokuwa imeanzishwa upya unaweza kutuma ombi la kubadilisha kazi ukitumia mfumo wa arifa wa kielektroniki wa MoL.

## Je, ninaweza kughairi ombi langu la kubadilisha kazi?

Ikiwa umetuma ombi la kubadilisha kazi kupitia mfumo wa arifa wa kielektroniki wa MoL na ombi lako bado linakaguliwa, unaweza kulighairi kupitia mfumo huo huo. Ingia kwenye mfumo wa arifa wa kielektroniki wa MoL ukitumia nambari yako ya QID na nambari yako ya simu.

Iwapo ungependa kughairi ombi lako la kubadilisha kazi baada ya kupokea kibali kutoka kwa Wizara na kabla ya mkataba wako mpya wa ajira kuthibitishwa, unahitaji kutuma barua iliyotiwa saini kwa Kiarabu iliyotumwa kwa Mkuu wa Idara ya Mahusiano ya Kazi ikiomba kughairi ombi lako. Katika barua, unapaswa kujumuisha maelezo mafupi kwa nini unaomba kughairi ombi lako pamoja na nambari ya EC, nakala ya QID yako na nambari ya simu ya mkononi.

## Je, ninaweza kupata mafao yangu ya mwisho wa huduma ikiwa nitabadilisha mwajiri?

Ikiwa umemaliza angalau mwaka mmoja wa ajira na unataka kubadilisha mwajiri, una haki ya kupokea kutoka kwa mwajiri wako wa sasa mafao yako ya mwisho wa huduma pamoja na likizo yoyote ya mwaka iliyoongezeka na mafao mengine kama ilivyoelezwa katika mkataba wako wa ajira.

## Ikiwa sijalipwa mishahara yangu, je, bado nitalazimika kutoa notisi kabla ya kubadilisha kazi?

Ikiwa mwajiri wako wa sasa hajatimiza wajibu wake wa kisheria (ikijumuisha na malipo ya mishahara), basi unaweza kubadilisha kazi bila kutoa notisi yoyote kulingana na Kifungu kilichorekebishwa cha 51 cha Sheria ya Kazi. Unapaswa kutuma lalamiko kwa Idara ya Mahusiano ya Kazi ya MoL.Unaweza kufanya hivyo kupitia Malalamiko na Wakosoaji wa Serikali la Wizara.

Kumbuka una haki kamili ya kupata mishahara yako unayodai, bakshishi ya mwisho wa huduma (baada ya zaidi ya mwaka mmoja wa huduma) sawia na likizo yoyote ya mwaka unayodai. Mwajiri wako atalazimika kulipia gharama ya tikiti ya ndege ili urudi nchini kwako ikiwa utachagua kuondoka Qatar.

## Je, ninaweza tu kuondoka Qatar na kurudi tena kuanza kazi mpya?

Ukiondoka Qatar bila kutoa arifu au kumaliza kipindi chako cha notisi, hautaweza kurudi kufanya kazi nchini Qatar kwa mwaka mmoja. Ili kuepukana na hali kama hiyo, unapaswa kufuata taratibu zilizo hapa chini:

Ikiwa unataka kuondoka Qatar wakati wa kipindi chako cha majaribio:

- Unapaswa kumjulisha mwajiri wako kupitia mfumo wa arifa wa kielektroniki wa MoL. Kipindi cha notisi kinapaswa kukubaliwa na mwajiri wako lakini hakipaswi kuwa zaidi ya miezi miwili.
- Ikiwa unataka kuondoka bila kumaliza kipindi chako cha notisi, unapaswa kulipa fidia kwa mwajiri wako sawa na mshahara wako wa msingi kwa sehemu iliyobaki ya kipindi cha notisi, ilimradi kiasi hiki cha pesa hakizidi mishahara ya msingi ya miezi miwili.

Ikiwa unataka kuondoka Qatar baada ya kipindi chako cha majaribio:

- Ikiwa umefanya kazi na mwajiri kwa miaka miwili au kwa muda usiozidi huo, unapaswa kumjulisha mwajiri wako mwezi mmoja kabla ya usitishaji wa mkataba wa ajira, kupitia mfumo wa arifa wa kielektroniki wa MoL.
- Ikiwa umefanya kazi na mwajiri kwa zaidi ya miaka miwili, lazima umjulishe mwajiri wako miezi miwili kabla ya usitishaji wa mkataba wa ajira, kupitia mfumo wa arifa wa kielektroniki wa MoL.
- Ikiwa unataka kuondoka Qatar bila kuzingatia kipindi cha notisi hapo juu, unapaswa kumlipa mwajiri fidia sawa na mshahara wako wa msingi kwa sehemu iliyobaki ya kipindi cha notisi.

## Je, mwajiri wangu anaweza kusitisha mkataba wa ajira?

Ndio, mwajiri wako anaweza kusitisha mkataba wako wa ajira.

1. **Wakati wa kipindi cha majaribio,** mwajiri wako akiona "hufai kutekeleza majukumu yako ya kazi" kama ilivyoainishwa katika mkataba wako wa ajira, mwajiri wako anaweza kusitisha mkataba lakini lazima akujulishe angalau mwezi mmoja kabla ya usitishaji kupitia mfumo wa kielektroniki wa MoL.

   Ikiwa baada ya usitishaji wa mkataba wa ajira unaamua kurudi katika nchi unayoishi, mwajiri lazima alipie gharama za tikiti ya ndege ya kurudi.

1. **Baada ya kipindi cha majaribio,** ikiwa mwajiri wako anataka kusitisha mkataba wako wa ajira lazima akujulishe kupitia mfumo wa kielektroniki wa MoL.
   - Ikiwa umefanya kazi na mwajiri kwa miaka miwili au kwa muda usiozidi huo, kipindi cha notisi ni mwezi mmoja.
   - Ikiwa umefanya kazi na mwajiri kwa zaidi ya miaka miwili, kipindi cha notisi ni miezi miwili.

Wewe na mwajiri wako lazima mdumishe sheria na masharti ya mkataba wa ajira wakati wa kipindi cha notisi.

## Je, mwajiri wangu anaweza kusitisha mkataba wangu wa ajira bila kuzingatia kipindi cha notisi?

Ikiwa mwajiri atasitisha mkataba wako bila kuzingatia kipindi cha notisi, lazima akulipe fidia sawa na mshahara wako wa msingi kwa kipindi cha notisi au sehemu iliyobaki ya kipindi cha notisi.

Kwa mfano: Ikiwa mshahara wako wa msingi ni QAR 1,500 kwa mwezi na mwajiri wako akikuomba uache kufanya kazi wiki mbili kabla ya kumalizika kwa kipindi cha notisi cha mwezi mmoja mwajiri wako atalazimika kukulipa QAR 750 kusitisha mkataba kisheria.

## Je, mwajiri wangu lazima alipe tikiti ya ndege ya kurudi kwenye nchi ninayoishi baada ya usitishaji wa mkataba wa ajira?

Mwajiri wako lazima kukamilisha taratibu zako za kurudishwa nyumbani, ikiwa ni pamoja na kulipia gharama ya tikiti ya ndege ya kurudi katika nchi yako unayoishi ndani ya muda wa kiwango cha juu wa wiki mbili kutoka kumalizika kwa mkataba wako. Ukijiunga na mwajiri mwingine kabla ya kuondoka nchini, wajibu wa kurudishwa nyumbani utakuwa wa lazima kwa mwajiri mpya.

Katika kesi ambazo utasitisha mkataba na unapanga kuondoka Qatar, huku ukiheshimu kipindi cha notisi (nje ya wigo wa Kifungu kilichorekebishwa cha 51 cha Sheria ya Kazi), mwajiri wako atalipa tu sehemu ya gharama ya tikiti ya ndege ya kurudi sawia na muda wa ajira uliomaliza kwa muda kamili wa mkataba. Kwa mfano: Ikiwa utasitisha mkataba wako wa ajira wa miaka miwili baada ya kufanya kazi mwaka mmoja, mwajiri atalipa nusu ya gharama yote ya tikiti ya ndege ya kurudi.

## KWA WAFANYAKAZI AMBAO SHERIA MAALUM INAWAHUSU

### Je, ni sheria zipi za kusitisha na kubadilisha kazi kwa wafanyakazi wa ndani?

Sheria za kusitisha na kubadilisha kazi kwa wafanyakazi wa ndani ni sawa na zile za wafanyakazi katika sekta binafsi, ambao Sheria ya Kazi Namba. 14 ya 2004 inawahusu. Mkataba wa kawaida wa ajira uliosasishwa kwa ajili ya wafanyakazi wa ndani unaoonyesha sheria hizi tayari unatumika. Hata hivyo, kumbuka kwamba kipindi cha majaribio kwa wafanyakazi wa ndani hakitazidi miezi 3. Vilevile, mfanyakazi wa ndani anaweza tu kuwa na kipindi kimoja na mwajiri yule yule.

Waajiri wa wafanyakazi wa ndani wanaweza kusitisha upande mmoja wa mkataba wa ajira bila notisi na bila kutoa bakshishi ya mwisho wa huduma kwa mwaka wa kufukuzwa kazi, ikiwa mfanyakazi hatii wajibu ulioainishwa katika mkataba wa ajira au yale yaliyoelezwa katika Vifungu 11 na 16 vya Sheria Namba. 15 vya 2017 juu ya Wafanyakazi wa Ndani.

Zaidi ya hayo, kesi zilizotajwa na Kifungu 17 cha Sheria Namba. 15 cha 2017 juu ya Wafanyakazi wa Ndani, wafanyakazi wa ndani wanaweza kusitisha upande mmoja wa mkataba wakati wowote wa kipindi cha mkataba bila notisi na huku wakiendelea kuweka haki yao ya bakshishi ya mwisho wa huduma, sawia na ada za likizo ya mwisho wa mwaka na pia tikiti ya ndege ya kurudi nchini yake ya asili.

### Ni sheria zipi za kusitisha na kubadilisha kazi kwa wafanyakazi wa kilimo na malisho ya mifugo, na wavuvi?

Sheria za kusitisha na kubadilisha kazi kwa wafanyakazi wa kilimo na malisho ya mifugo, na pia wavuvi, ni sawa kabisa na zile za wafanyakazi wa sekta binafsi ambao Sheria ya Kazi Namba. 14 ya 2004 inawahusu.

Ikiwa unahitaji maelezo zaidi, angalia Baraza la Azimio la Mawaziri Namba. 17 la 2012 juu ya matumizi ya baadhi ya masharti ya Sheria ya Kazi Namba. 14 ya 2004 kwa wafanyakazi wa kilimo na malisho ya mifugo.

## NINAPASWA KUFANYA NINI IKIWA MWAJIRI WANGU WA SASA ANANIZUIA KUHAMIA KWA MWAJIRI MWINGINE AU NIKIHITAJI TAARIFA ZAIDI?

Ikiwa unahisi kuwa mwajiri wako wa sasa anakuzuia bila haki kubadilisha kazi au ikiwa unahitaji taarifa zaidi, wasiliana na Idara ya Mahusiano ya Kazi ya Wizara ya Kazi kwenye simu ya moja kwa moja (**40288101**), kwa barua pepe (info@mol.gov.qa), au tembelea ofisi zetu. Pia unaweza kutuma lalamiko kwa Wizara kwa kutumia Jukwaa La Pamoja la Malalamiko na Wakosoaji wa Serikali la Wizara kutuma lalamiko.